# MAANDALIZI YA KUSTAAFU

PROF E.T. BISANDA

OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

# UTANGULIZI

- Maisha yetu yana hatua tatu muhimu
  - Kukua na kupata elimu na ujuzi
  - Kufanya kazi
  - Kustaafu
- Miaka ya kufanya kazi ya ajira ni kati ya 18 na 60 au 65
- Hata ajira inapokoma, na mtu kustaafu, bado mtu anaweza kuishi hadi umri wa miaka 90 au zaidi kabla ya kupumzika kaburini

# HALI HALISI YA WASTAAFU

- Wengi hawapati fursa mpya kufanya kazi hata kwa mkataba ingawa bado wana nguvu
- Wengi bado wana wategemezi, kama watoto wanaosoma shule, kulea wazazi ambao ni wazee zaidi
- Wengi wanasumbuliwa na maradhi mbalimbali yasiyoambukizwa (presha, kisukari, tezi, kiharusi, mifupa, macho, meno, n.k.).
- Wanakaa muda mwingi bila kazi, hawana usingizi, wana mawazo mengi, dunia inaenda kasi zaidi, hofu kugongwa na magari, n.k
- Hawana yale mapato waliyozoea, na watoto kuwaona mzigo usiobebeka!
- Heshima waliyozoea haipo kwa vile hawana pesa.

# KIPINDI CHA MATESO?

- Miaka hii 30 na ziada, ni muda ambao umeleta mateso kwa watu wengi waliostaafu, kutokana na kipato kidogo (pensheni).
- Hata dreva haruhusiwi kuendesha gari la abiria au la umma baada ya kustaafu
- Brela haikubali kusajili wakurugenzi wa makampuni wakikikia umri wa miaka 70

# KIINUA MGONGO

- Wastaafu wengi wanapata kiinua mgongo (lumpsum) pale wanapostaafu, na pensheni kila mwezi kutegemea na ajira zao.
- Kuna wengine wanapostaafu wanakuwa hawajajenga nyumba, hivyo kiinua mgongo kutumika kupata makazi!
- Baada ya muda mfupi kiinua mgongo huisha, na mstaafu hupata wakati mgumu na msongo wa mawazo.

# KWA NINI MAANDALIZI?

- Unapofikiria kustaafu, jiulize maswali haya:
  - Nitastaafu lini?
  - Je nitakuwa na akiba ya kutosha nikistaafu?
  - Je? Mali yangu itadumu kwa muda mrefu?
  - Mke/Mume wangu ataweza kujimudu nikiondoka?

# MAANDALIZI: USISUBIRI KIINUA MGONGO

- Ni vema mfanyakazi kuanzisha mradi wa kumletea kipato mapema kabla ya kustaafu. Wekeza kabla ya kustaafu. Watoto siyo akiba ya uzeeni!
- Fedha za kiinua mgongo unapaswa kuwa mtaji wa kuboresha mradi, na siyo kuanza mradi.
- Mfanyakazi ajitahidi kuwa na makazi ya kustaafu (mjini au kijijini) kabla ya kustaafu.
- Mfanyakazi aandae mpango mahususi wa maisha yake pindi akistaafu, unaoonyesha: ataishi wapi? Atajishughulisha na nini?
- Uwe na nyumba mjini unayoweza kupangisha ukapata pesa

# ANZA KUJIWEKEA AKIBA

- Ratibu mali zako na Matumizi
  - Je mapato yako yanazidi matumizi yako?
  - Je una madeni katika mabenki unayolipa kwa mshahara wako?
- Wekeza katika maeneo tofauti.
  - Usiweke mayai yako yote katika kapu moja
  - Wekeza katika kilimo, ufugaji, viwanda, masoko ya mitaji, n.k.

# KIKOKOTOO

- Unapostaafu unapewa asilimia 33 ya michango yako katika mifuko ya pensheni.
- Asilimia 67 inawekwa kwa ajili ya kukupatia pensheni kila mwezi.
- Haijalishi utaishi miaka mingapi baada ya kustaafu. Mara kwa mara utatakiwa kuthibitisha kuwa bado uko hai.

# KUISHI MJINI BAADA YA KUSTAAFU

- Wengi tumefanya kazi na kuuzoea mji.
- Marafiki zetu wengi wapo mjini
- Nyumba tumejenga mjini
- Mjini kuna huduma nzuri za maji, umeme, hospitali, barabara, n.k.
- Watoto wetu wako mjini
- Hivyo, wastaafu wengi hubakia mijini wakisubiri kifo.

# LAKINI ......

- Wastaafu wengi hawana cha kufanya mjini, ila labda kucheza bao, n.k.
- Kukosa kazi, hata kama una mapato ya kutosha kwenye miradi uliyowekeza, inaweza nayo kuwa shida kwa waliozoea kazi!
- Matumizi ya mjini huwa yanapanda haraka, wakati pensheni haiongezeki kwa kasi hiyo.
- Wastaafu wana shida kutembea barabarani, tokana na wingi wa magari, na kupungua uwezo wao wa kuona na kusikia!

# KUISHI KIJIJINI BAADA YA KUSTAAFU

- Maisha ya kijijini yanamfanya mtu kuwa busy muda wote
- Lakini, siyo wote wamezoea maisha ya kilimo na ufugaji, inahitaji uthubutu mkubwa...
- Ukistaafu kwenda kijijini kwenu, utajikuta....
  - Huna marafiki waliobaki hai
  - Waliopo wanakuona wewe una fedha, na utapata wategemezi wengi kula pensheni yako....
  - Hujazoea shida za kijijini, kuchota maji, umeme, usafiri, n.k.

# MAISHA BAADA YA KUSTAAFU

- Una miaka 30 au zaidi ya kuishi baada ya kustaafu
- Tunza afya yako, fanya mazoezi, kula vizuri, epuka vyakula vya hovyo
- Jifunze stadi mpya, ikibidi nenda chuo, ujipe maarifa mapya yatakayokusaidia kuwa mjasiriamali
  - Ufugaji wa nyuki, ufugaji wa kuku, n.k
  - Kilimo cha bustani, n.k.

- Ikiwezekana, usiishi katika mji mkubwa.  Kipato chako kidogo, hakitahimili ongezeko la haraka la gharama za maisha katika miji mikubwa
- Fuga mbuzi, kuku, na panda miti ya matunda.  Vitakupa fedha kidogo, na kusaidia lishe yako.
- Usitumie pesa zaidi ya mapato yako, hata kwa watoto.
- Huu ni wakati wako kufaidi jasho lako na mke wako.
- Usitegemee sana kuwa watoto watakusaidia. Shukuru sana kama wanaweza kukutunza.
- Jishugulishe katika mambo ya kanisa (uinjilisti, uimbaji, semina, vyama, n.k.), lala vizuri, fanya mazoezi madogo kama kutembea, yakubali mabadiliko katika maisha yako na mazingira yako.

# MWISHO

- Samehe na kusahau: huu siyo muda wa kuwaza wale waliokukosea, waliokudhulumu, n.k. Vitakupa msongo na presha bure.
- Chukua maisha kama yalivyo. Jua siku moja utaiaga dunia. Huu ni wakati wa kuwa karibu na Mungu wako.
- Tumia wakati wako kuwaasa vijana. Watoto wako, wajukuu wako, majirani, n.k. Ipo siku nao watakuwa wazee na wastaafu, ili wasirudie makosa uliyofanya.